# 8 SHULE YA KANYAMEDHA

## MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA

## KISWAHILI

**JINA**: **NAMBARI YA USAJILI :** **DARASA:**

### A. UFAHAMU (Alama 10 )

(a) **Soma kifungu hiki cha ufahamu.**

Sali aliketi kando ya barabara iliyoelekea mjini. Alisoma maandishi HAKI NA UKWELI kwenye trela ambalo lilikuwa linapita. Aliyaona maandishi hayo kama ishara nzuri ya matumaini katika maisha yake. Aliiangalia barabara hiyo kwa tuo zaidi. Aliona mabonde na milima ambayo iliwakabili wasafiri. Baadhi ya magari yalishindwa kupanda milima na kujikokota kama konokono. Aliyalinganisha maisha yake na magari hayo.

Aliyaangalia magari hayo na kujiangalia. Machozi yalimtiririka njia mbilimbili kwenye uso wake. Matone mengine yalikiangukia kifua chake. **Alilia kwi kwi kwi.** Alipangusa machozi hayo harakaharaka. Aliyaangalia tena magari yale yaliyokuwa yanajikokota. Mengine yalikuwa yamefanikiwa kupanda mlima na kuifikia sehemu tambarare. Yalikuwa yanashika kasi. "Hivi kumbe maisha ni panda shuka." Sali alijiliwaza.

Sali alikumbuka alikotoka. Huko kulikuwa na giza totoro. Alikumbuka ajali iliyotokea mwezi wa sita kwenye barabara iyo hiyo na kuwachukua wavyele wake akiwa **kikembe**. "Ama kweli maisha ni kitendawili. Barabara hii iliyonisababishia **simanzi** na kilio kisicho kifani ndiyo itakayoniletea furaha na kicheko leo." Sali alijisemea.

Wazazi wa Sali walipoupungia ulimwengu mkono wa buriani, alibaki yatima. Lililokuwa limebaki ni kukesha na kuomba dua kwa Maulana amjalie **mbawazi** ili aweze kuendelea na maisha na elimu yake.

Sali alichukuliwa na mjomba wake Dori. Dori alimuahidi kuwa angempa usaidizi kwa hali na mali. Sali hakuwa wa hulka mbaya, kwa hivyo mjomba Dori alimpenda na kumtunza kama mwanawe. Kwa upande mwingine, mkewe Dori alimchukia na kumtesa Sali. Alimfanyisha kazi za sulubu, kumpimia chakula na wakati mwingine kumchelewesha Sali kwenda shuleni. Kusudi lake lilikuwa kumhini Sali fursa ya kujiendeleza kielimu. Mjomba Dori alipodadisi mambo haya, bibi yake alimjibu kwa ukali, "Unampendelea Sali, utamharibu mtoto wa dadako. Sali ni mtoto wa kike, lazima apike, aoshe nguo na asafishe nyumba. Kumbuka kuwa mchelea mwana kulia, hulia yeye." Mjomba alisema, "Si lazima majukumu haya mazito yafanywe na mtoto wa kike. Kila mtoto anafaa kujifunza kufanya haya yote kwa kadri. Kumbuka Sali bado ni mtoto."

Baada ya kuchunguza, Dori aligundua kuwa mkewe alikuwa akimdhulumu Sali. Aliamua kumpeleka Sali mjini kwa dadake mdogo.

Sali aligutushwa na mlio wa honi la gari la Dori. Alinyanyuka kwa furaha kuingia garini. "Shangazi yako anakusubiri kwa hamu na ghamu. Atahakikisha kuwa utapata muda wa kuendeleza elimu yako. Tayari amekutafutia nafasi katika shule ya Melo." Dori alisema.

"Asante mjomba Dori. Najua unanijali. Nitajitahidi ili nifaidi." Sali alimwambia mjomba wake.

Baada ya muda, mkewe Dori alijihisi mpweke. Alimtamani Sali. Aliamua kufunga safari kwenda kumtembelea Sali mjini. Alipofika, Sali alimkaribisha kwa moyo mkunjufu. Aligundua kuwa afya ya Sali imeimarika na amekuwa mchangamfu zaidi. Aliambiwa kuwa Sali alikuwa ameonyesha umahiri shuleni na kuwa kipenzi cha wengi. Bibi yake Dori alimwambia Sali, "Tafadhali nisamehe. Nimegundua nilikukosea. Naomba uwe ukinitembelea mara kwa mara." Sali na mke wa Dori walidondokwa na machozi ya furaha huku wakikumbatiana.